

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
11 Oktoba 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Bashiri Rashidi
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
George Kabogo
Husein Hamza Hamisi
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Alex
Mussa Omari
Ramadhani Rajabu Nyengo
Shamte J Kigoma

Msafara wa Baisikeli

Wakati wa wiki Elaine alitumia badjeti kwa ubalozi wa Ireland, walikubali, walitutumia mkataba na Elaine alisaini kwa ajili ya UWABA, Filbert aliwaletea mkataba na alipokea hundi na Paulo aliweka hundi kwenye benki. Itachukua masiku kabla hela ipo tayari kuchukua. Wiki ijayo Mejah na Elaine wataenda benki kuchukua hela. Halafu Hussein Hamza atasaidia kununua baisikeli, kutoka godown Nyerere Road, Sosthenes alisema kwa simu atatengeneza mabango na Edgar atatayarisha T-shirts.

Elaine aliwapigia simu kampuni ya guta na walisema tupigie tena jumatano kwa sababu mtu anayehusika atakuwa amerudi. Pia wanatengeneza baisikeli za walemavu.

Elaine alimpigia simu Bwana Lawrence wa Bakhresa tena. Alisema alimpa Bwana Bakhresa barua yetu lakini hakuna jibu bado. Kassim Bakari atafuatalia wiki hii kwa kutembelea ofisi.

Elaine alipigia simu Ultimate Security na walisema watapenda kusaidia lakini ataongea na wafanyakazi wenzake na tuwapigie simu tena kuwakubusha.

Filbert alipeleka barua kwa Diwani Lupilya na Manispaa ya Ilala yenyewe kuomba Mnazi Mmoja bure. Atafuatalia tena jumatatu.

Elaine aliandaa barua za mwaliko. George atapeleka kwa Kali Mata jumatatu asubuhi. Filbert atapeleka kwa meya wa Ilala, Chuo cha Usafirishaji, Meya wa Jiji, Wizara ya Mambo ya Ndani.. Edgar atapeleka kwa Meya wa Kinondoni, Tanzania Coalition for Sustainable Development, SUMATRA. Hussein Hamza atapeleka kwa Meya wa Temeke. Bashiri atapeleka kwa shirika la walemavu na Haki Elimu. Ally Athman atapeleka kwa mradi wa DART. Paulo, Elaine na Mejah watapeleka zingine.

Mejah alituma ujumbe kwamba Business Times wataweka tangazo bure.

Elaine alileta mabango na vipeperushi. Wanachama walichukua moja moja na watafanya photocopy na watadai hela wiki ijayo. Pia zingine zinaenda pamoja na barua za mwaliko. Elaine alitumia Tsh 10,000 kufanya photocopy na atadai wakati tunachukua hela kutoka benki.

Watafiti

Filbert alikutana na watafiti na aliwapa savei. Sasa wameondoka nchi.

Mkutano na Allan Jones na mambo kufuatalia

Jumatatu Elaine, Filbert, Hussein Hamza, Paulo na Bashiri walikutana na Allan Jones. Elaine aliandika dondoo na masuala ya muhimu kufuatalia ni kama yafuatayo:

Aliomba samahani kuhusu jinsi tulivyodharau tulipotembea Wizara ya Miundumbinu idara ya usalama barabarani.

Kuna tukio la usalama barabarani Morogoro na anapenda tuhudhurie kufundisha wanafunzi wa shule kuhusu usalama wa baisikeli. Filbert, Bashiri na Edgar walichaguliwa kuhudhuria. Tulitandaa badjeti na Elaine atamtumia kwa email – jumla ni Tsh 230,000.

Pia alituambia kuhusu mkutano Bagamoyo kuhusu sekta ya usafiri na tuliomba nafasi ya wanachama wa UWABA kuhudhuria siku ya Dar es Salaam (alhamisi) na aliongea na idara yake akapata nafasi kwa mwanachama mmoja. Mejah alihudhuria na atatupa taarifa wiki ijayo.

Mambo ya hela

Filbert alitumia Tsh 1,000 kukodi baisikeli siku alipeleka barua. Tulipata Tsh 7,000 ya kodi ya guta kutoka kwa Ally Saidi Mwishehe – bado tunam dai wiki mbili. Juma alimpa Juma Chibaya Tsh 38,000 ya advance ya kodi ya ofisi. Juma anabaki na Tsh 27,200 ya hela ya UWABA.

Guta inahitaji ringi mpya na Juma alikubali kumpa hela Ally Saidi Mwishehe kwa ajili ya kununua.